



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI JULAI NA AGOSTI, 2026

1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha miezi ya Julai na Agosti, 2026 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi, ikiambatana na hali ya baridi ya wastani hadi baridi kali, hususani nyakati za usiku na alfajiri. Aidha, vipindi vifupi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, vikiambatana na mawimbi makubwa katika bahari na maziwa makuu.

Hali hizi ziliashiria kuendelea kwa msimu wa Kipupwe (Juni – Agosti) 2026, na mifumo ya hali ya hewa iliyojitokeza pamoja pamoja na athari zake imeendana na taarifa za mwelekeo wa mvua za msimu zilizotolewa hapo awali.

2.0 JULAI 2026

2.1 Mvua kubwa

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2026 maeneo mengi ya nchi yaliendelea kukumbwa na hali ya ukavu kwa kiasi kikubwa, huku vipindi vya mvua nyepesi hadi za wastani vikijitokeza katika maeneo machache. Hakuna kipindi cha mvua kubwa ($\geq$ milimita 50) kilichorekodiwa katika mwezi huu. Kiwango kikubwa zaidi cha mvua ndani ya saa 24 kilikuwa milimita 13.4 kilichorekodiwa katika kituo cha Tanga mnamo tarehe 7 Julai 2026.

2.2 Hali joto

Katika kipindi cha mwezi Julai 2026, hakuna ripoti ya vipindi vya joto kali vilivyorekodiwa nchini. Aidha, kiwango cha zaidi cha joto cha nyuzi joto 33.7 °C kilirekodiwa katika kituo cha Ibadakuli, mkoani Shinyanga mnamo tarehe 19 Julai 2026.

Kwa upande mwingine, hali ya baridi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na kanda ya kusini. Kiwango cha joto la chini zaidi cha nyuzi joto 4.6 °C kilirekodiwa katika kituo cha Uyole (mkoa wa Mbeya) tarehe 25 Julai, ikifuatiwa na nyuzi joto 5.0 °C na 5.2 °C vilivyorekodiwa katika vituo vya Uyole na Igeri tarehe 2 na 28 Julai 2026 mtawalia. Katika kipindi chote cha mwezi, kituo cha Uyole kilirekodi joto la chini la nyuzi 10 au chini yake kwa takribani siku ishirini na tano (25), wakati kituo cha Igeri kilikumbwa na hali kama hiyo karibu kila siku ya mwezi (siku 31).

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:


Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Jedwali 1: Idadi ya siku zenye joto la chini la nyuzi 10 au chini yake kwa mwezi wa Julai 2026

Kanda	Kituo	Idadi ya Siku ($\leq 10^{\circ}\text{C}$)	Kiwango cha chini zaidi kurekodiwa ($^{\circ}\text{C}$)
Nyanda za Juu kusini Magharibi	Igeri	31	5.2 $^{\circ}\text{C}$
	Uyole	25	4.6 $^{\circ}\text{C}$
	Mbozi	21	6.8 $^{\circ}\text{C}$
	Iringa	3	8.6 $^{\circ}\text{C}$
	Sumbawanga	9	8.6 $^{\circ}\text{C}$
Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki	Arusha	1	9.6 $^{\circ}\text{C}$
Kanda ya Kusini	Songea	4	9.2 $^{\circ}\text{C}$

Kielelezo 1 kinaonesha mwenendo wa joto la chini la kila siku katika vituo vya Uyole na Igeri kwa mwezi Julai 2026. Mwenendo huo unaonesha kuwa hali ya baridi iliendelea kutawala katika wiki ya kwanza ya Julai, ikifuatiwa na ongezeko dogo la joto la chini katika wiki ya pili ya mwezi.



Kielelezo 1: Mwenendo wa joto la chini katika vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi Julai 2026

2.3 Upepo Mkali

Katika kipindi cha mwezi Julai, vipindi vifupi vya upepo mkali unaofika au kuzidi kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan katika ukanda wa

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

pwani (Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara, na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Shinyanga na Mwanza), kanda ya kati (mikoa ya Singida na Dodoma) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Iringa na Songwe).

Nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali ikiwemo kusambaa kwa vumbi, kupeperushwa kwa takataka na kusababisha kupungua kwa uono. Maeneo machache ya mwambao wa pwani ya bahari na maziwa makuu yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini na ziwani sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika maeneo hayo.

3.0 AGOSTI 2026

3.1 Mvua Kubwa

Katika kipindi cha mwezi Agosti 2026, vipindi vya mvua nyepesi hadi za wastani vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan katika ukanda wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo ya juu ya nyanda kaskazini mashariki. Matukio machache ya mvua kubwa pia yalirekodiwa katika mwezi huu. Kiwango kikubwa zaidi cha mvua ya siku moja kilirekodiwa katika kituo cha Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, ambapo milimita 53.4 zilinyesha tarehe 21 Agosti, ikifuatiwa na milimita 23.2 zilizorekodiwa katika kituo hicho hicho tarehe 22 Agosti 2026.

3.2 Hali joto

Katika mwezi Agosti 2026, hakuna viwango joto kali la juu vilivyorekodiwa nchini. Joto la juu zaidi lilikuwa nyuzi joto 33.3 °C, lililorekodiwa katika kituo cha Mpanda (mkoani Katavi) tarehe 11 Agosti, likifuatiwa na nyuzi joto 33.1 °C na 32.9 °C katika vituo vya Katavi na Ibadakuli (mkoani Shinyanga) tarehe 10 na 22 Agosti 2026 mtawalia.

Kwa upande mwingine, katika baadhi ya maeneo, hususan katika nyanda za juu za kusini magharibi, ambako hali ya baridi ya wastani hadi kali ilitawala. Joto la chini zaidi la nyuzi 5.0 °C lilirekodiwa katika kituo cha Uyole (mkoani Mbeya) tarehe 2 Agosti, likifuatiwa na nyuzi 5.5 °C zilizorekodiwa katika kituo cha Igeri siku hiyo hiyo. Jedwali 2 hapa chini linaonesha kwa kina idadi ya siku ambazo kila kituo kilirekodi joto la chini la nyuzi 10 °C au chini yake.

Jedwali 2: Idadi ya siku ambazo vituo vilirekodi joto la chini la nyuzi 10 au chini yake katika mwezi wa Agosti 2026

Kanda	Kituo	Idadi ya Siku ($\leq 10^{\circ}\text{C}$)	Kiwango cha chini zaidi kurekodiwa ($^{\circ}\text{C}$)
Nyanda za Juu Kusini Magharibi	Igeri	30	5.5 °C
	Uyole	16	5.0 °C
	Mbozi	12	7.3 °C
	Iringa	3	8.9 °C
	Sumbawanga	1	9.3 °C
Nyanda za Juu	Arusha	4	8.8 °C


Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Kaskazini Mashariki			
Kanda ya Kusini	Songea	4	9.2°C

Kielelezo 2 kinaonesha mwenendo wa joto la chini katika vituo vya Uyole na Igeri kwa mwezi Agosti 2026. Mwenendo huo unaonesha kuwa hali ya baridi iliendelea kutawala katika mwezi mzima, hususan wiki ya kwanza na ya tatu. Hata hivyo, kituo cha Igeri kilikumbwa na siku nyingi zaidi za baridi ukilinganisha na maeneo mengine, kikiwa na siku 30 za joto la chini la nyuzi 10 °C au chini yake.



Kielelezo 2: Mwenendo wa joto la chini katika vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi Agosti 2026.

3.3 Upepo Mkali

Kuimarika kidogo kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini ilisababisha vipindi vifupi vya upepo mkali wa kusi, unaofikia au kuzidi kilomita 40 kwa saa, katika baadhi ya maeneo nchini, hususan katika ukanda wa pwani (Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, na visiwa vya Unguja na Pemba), mikoa ya kati (Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Iringa na Songwe) na maeneo yanayozunguka ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Mwanza na Shinyanga). Vipindi hivyo vya upepo vilisababisha madhara na kuvuruga shughuli za usafiri wa majini katika bahari na maziwa makubwa.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira.

Imetolewa: tarehe 10 Septemba, 2026

Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)